**Kuwezesha Sayansi ya Mazingira Barani Afrika: Ruzuku ya Utafiti ya Jennifer Ward Oppenheimer (JWO) Inatafuta Mpokeaji Mwingine Shupavu wa Ruzuku**

Kihistoria, bara la Afrika limewakilishwa kwa kiwango cha chini katika juhudi za utafiti na maendeleo ya kimataifa, hali hii inaandamana na rasilimali chache zilizotengewa mipango ya utafiti ikilinganishwa na maeneo mengine. Hata hivyo, kuna utambuzi unaoendelea kukua wa maoni kuhusu uwezekano mkubwa wa uvumbuzi na maendeleo ya kisayansi katika mandhari mapana ya Afrika na jamii mbalimbali za Afrika. Kutokana na haya, hii ndiyo sababu ruzuku za utafiti kama vile Ruzuku ya Utafiti ya Jennifer Ward Oppenheimer, ambayo sasa iko katika mwaka wake wa sita, ina athari nzuri.

Ruzuku ya Utafiti ya Jennifer Ward Oppenheimer (JWO Grant) ilianzishwa mwaka wa 2019 ili kuheshimu kazi na sifa za marehemu Jennifer Ward Oppenheimer, mwanaelimu mwanzilishi katika elimu barani Afrika na sayansi ya mazingira. Ruzuku ya Utafiti ya JWO imekuwa muhimu katika kuendeleza mipango muhimu ya utafiti katika bara zima. Inapokaribia mwongo mmoja wa kuwepo kwake, Ruzuku ya JWO inalenga kuvutia idadi kubwa zaidi ya wanasayansi wanaoanza taaluma yao ya kisayansi kutuma maombi ya ufadhili mwaka wa 2024, na kuwapa fursa ya kupokea tuzo hii yenye kuleta mabadiliko.

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, wasomi wanaonza taaluma yao ya sayansi na wanasayansi waliobobea katika taaluma mbalimbali za kimazingira kama vile bayoanuwai, plastiki ndogo, na vienezaji vya magonjwa wametafuta ruzuku hii kwa shauku ya kuchunguza mada bunifu za utafiti zinazolenga kushughulikia changamoto za kipekee zinazokabili mazingira asilia ya Afrika. Dk. Duncan MacFadyen, Mkuu wa Kitengo cha Utafiti na Uhifadhi cha Oppenheimer (Oppenheimer Generations Research and Conservation) , anasifu ruzuku hii ya Utafiti ya JWO kwa kuonyesha mawazo ya kisayansi ya kisasa, tafiti za kisayansi zenye ubunifu na kutoa jukwaa la kukuza na kusaidia akili bunifu za bara la Arika. Ruzuku hii pia inachangia kuleta sauti za Afrika katika mazungumzo ya kimataifa kuhusu mazingira na uendelevu.

Utafiti huu wa kisasa hautoi tu mwanga kuhusu masuala muhimu ya mazingira lakini pia unachangia kikamilifu katika kuleta mitazamo ya Kiafrika katika mijadala ya kimataifa kuhusu uendelevu. Mwaka jana, Dkt. Lovanomenjanahary Marline, mwanabrayafaiti mashuhuri kutoka Madagaska, alionyesha athari ya ruzuku kwa kupata $150,000 kwa utafiti wake msingi na wa kipekee. Utafiti wa Dkt. Marline kuhusu brayafaiti na licheni unachunguza uwezekano wao katika kufuatilia hatari kubwa za kimazingira na afya ya binadamu kama vile kupotea kwa bayoanuwai, mabadiliko ya hali ya hewa, na uchafuzi wa hewa. Kwa msaada wa Ruzuku ya Utafiti ya JWO, Dkt. Marline anashirikiana na watafiti na wanafunzi kutoka kote barani Afrika kuendeleza utafiti wake.

Athari chanya za Ruzuku ya Utafiti ya JWO zimewafikia wengi tangu kuanzishwa kwake,huku mwanasayansi aliyechapishwa Dkt. Haley Clements akiwa mpokeaji wa kwanza wa mwaka wa 2019. Mradi wake ulioshinda wenye mada “Quantifying the

Biodiversity Planetary Boundary for Africa," ulilenga kushughulikia hitaji kubwa la kuangazia ukuaji endelevu, na kuzuia kuvuka mipaka ya upotezaji wa bayoanuwai, na kuangazia faida za jamii za kuwekeza katika mazingira asili. Dkt. Clements kwa sasa ni mwanasayansi wa mwingiliano taaluma za uhifadhi katika Chuo Kikuu cha Stellenbosch.

Dkt. Bernard Coetzee, Dkt Gideon Idowu na Dkt. Elizabeth le Roux walitunukiwa Ruzuku ya Utafiti ya JWO mnamo mwaka wa 2020, 2021 na 2022, mtawalia. Utafiti wa Dkt. Le Roux unalenga kuoanisha michakato ya kiikolojia na maisha ya jamii za maeneo husika licha ya kuwepo kwa ongezeko la kutengwa kwa maeneo yaliyohifadhiwa ya Kiafrika. Kwa msaada wa ruzuku hiyo, Dkt. Le Roux alifaulu kupima muunganisho unaofikiwa kwa kuwepo na mbinu mbalimbali za usimamizi wa nyanda za malisho ya mifugo.

Dkt. Gideon Idowu kutoka Nigeria, mshindi wa ruzuku hiyo mwaka wa 2021, anasisitiza umuhimu wa kuchunguza vichafuzi vya kemikali na plastiki ndogo katika mifumo ya maji safi ya Afrika. Utafiti wake wa kibunifu unaenea zaidi ya muktadha wa bahari ambao umechunguzwa zaidi, huku ukichunguza athari za muda mfupi na mrefu kwa afya ya binadamu.

Utafiti wa Dkt. Bernard Coetzee unalenga kuelewa athari za matumizi ya mwanga uliobuniwa na wanadamu kwa bara la Afrika na nafasi yake katika kueneza magonjwa yanayoenezwa na wadudu kama vile homa ya dengue, virusi vya Zika na malaria. Ruzuku ya Utafiti ya JWO ilimsaidia kuwezesha uchunguzi katika eneo hili muhimu lakini ambalo halijatafitiwa kwa kina, ambalo linaweza kuokoa maisha ya watu wengi.

Ruzuku ya JWO imebadilika na kuwa chanzo muhimu cha usaidizi kwa watafiti na watu binafsi waliojitolea kukuza Afrika iliyo bora zaidi, kiuchumi na kimazingira. Programu hii haileti tu mabadiliko chanya bali pia inawawezesha wanasayansi wanaoanza taaluma yao kushughulikia majanga ya mabadiliko ya anga yanayolikumba bara la Afrika sasa. Katika mwaka wake wa sita, JWO inatoa wito kwa wanasayansi wa Kiafrika wanaoanza taaluma yao kutuma maombi ya mapendekezo ya ufadhili na kuupa utafiti wao msingi wenye kuleta mabadiliko nafasi ya kuleta mabadiliko ya kudumu.

**Mahitaji ya Kupata Ufadhili**

1. Mtuma maombi ya ufadhili anapaswa kuwa mwanasayansi Mwafrika anayeanza taaluma yake na aliye na uhusiano thabiti na taasisi ya Kiafrika inayoaminika na anapendekeza kufanya utafiti katika bara la Afrika.
2. Ruzuku ya Utafiti ya JWO ya 2024 inahimiza maombi ya utafiti yenye mwingiliano taaluma yanayoonyesha uhusiano thabiti kati ya bayoanuwai na uhifadhi.
3. Mtuma maombi ya ufadhili lazima awe na digrii ya Uzamifu (PhD) na asiwe na zaidi ya miaka saba ya kazi na /au uzoefu wa utafiti baada ya kupata shahada yake (isijumuishe mapumziko ya kazi, pamoja na mapumziko yanayohusiana na majukumu ya kifamilia).

4. Taasisi lazima iwe na uwezo uliothibitishwa wa kusimamia ufadhili na inatumia mbinu bora za usimamizi wa ruzuku ya ufadhili wa kifedha.
5. Ushirikiano wa kitaasisi unaweza kuwa wa kitaaluma, kitafiti, serikali, Mashirika Yasiyo ya Serikali (NGO), au shirika la faida.

**Tuzo ya Ruzuku**

Ruzuku ya JWO ya 2024 ya $150,000 (USD) itatolewa kwa mtuma maombi ya ufadhili mmoja aliyefaulu. Ruzuku hii itasaidia mpango wa utafiti wa hadi miaka mitatu. Kutakuwa na maombi ya mapendekezo ya ufadhili kila mwaka

kwa maombi mapya (utafiti uliofadhiliwa hapo awali hautastahiki), na mpokeaji ruzuku atatangazwa kwenye Mkutano wa Utafiti wa Oppenheimer mnamo tarehe 10 Oktoba 2024.

Ili kutuma maombi ya kupata ruzuku ya ufadhili ya JWO, tafadhali fuata kiungo hiki - [https://jworesearchgrant.org/grant-application/](https://jworesearchgrant.org/grant-application/)

Muda wa kutuma maombi ya ufadhili umefunguliwa kuanzia tarehe 2 Aprili 2024 hadi tarehe 3 Mei 2024.

**Kuhusu Kitengo cha Utafiti na Uhifadhi cha Oppenheimer**

Timu ya Kitengo cha Utafiti na Uhifadhi cha Oppenheimer (Oppenheimer Generations Research and Conservation) inaendelea kuunda taasisi ya utafiti ya kiwango cha juu ambayo inashirikiana na watafiti wa kitaifa na kimataifa kufanya utafiti wa kisasa unaolenga kuchunguza sayansi asilia, hali inayohakikisha kuleta matokeo ya kihalisia na yenye athari nzuri. Timu hii wamejitolea kuendeleza zaidi, kupanua, na kukuza ukuaji wa programu na mitandao ya uhifadhi endelevu katika bara zima la Afrika.

Kwa maswali ya zaidi, tafadhali wasiliana na:
Cebisa Luzipho
Mkuu wa Mahusiano Mema na Mawasiliano Cebisa@orchardon25.co.za